...a kufanya uvuvi na ufugaji wa kisasa aliyoitoa Rais Samia Suluhu Hassan

# Ulega ataka wavuvi kuchangamkia fursa

Na MWANDISHI WETU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amewataka wavuvi kuchangamkia fursa iliyotolewa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya ugawaji wa maboti na vizimba, wafanye kazi zao kisasa na kuboresha maisha.

Ulega alisema hayo mkoani Mwanza jana, alipofanya ziara katika Soko la Samaki la Kimataifa la Kirumba, alipowatembelea wavuvi hao na kusikiliza na kutatua kero zinazowakabili.

Alisema fursa hiyo ya vifaa vya kisasa aliyoitoa Dk. Rais Samia, wakiitumia vizuri, watafanya uvuvi na ufugaji wa kisasa wa samaki aina ya sato ambao utasaidia Ziwa Victoria kupumua na kusababisha sangara na dagaa kuongezeka na kuinua uchumi wao.

"Tutumie fursa hiyo vizuri, tuzalishe vya kutosha, Rais Samia aone umuhimu wa kutuongeza vyombo vingine vya kisasa kwa sababu, anachokifanya ni kutuwekea mazingira mazuri, tuendelee kunufaika na shughuli zetu," alisema.

Kuhusu kero za tozo, Waziri Ulega, aliwataka wavuvi hao, kuwa na subira wakati jambo hilo linaendelea kufanyiwa kazi na mamlaka husika.

Hata hivyo, Ulega alimweleleza Mkurugenzi wa Uvuvi, Stephen Lukanga, kuhakikisha anaweka mikakati madhubuti ya kukomesha uvuvi haramu na kuhakikisha biashara ya mazao ya uvuvi, inafanyika katika masoko rasmi huku akimpa mwezi mmoja kutekeleza maagizo hayo.

## MAKABIDHIANO




MKURUGENZI wa Ubinafsishaji kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina, Mohamed Nyasama (kulia), akimkabidhi Kamishina wa Uhifadhi wa Mamlaka ya usimamizi wa Wanyama Pori Tanzania (TAWA), Mabula Nyanda, nyaraka za umiliki wa mashamba matatu ya Stain kuendeleza shughuli za uhifadhi na Utalii, katika Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha jana.(Picha na Lilian Joel).

Anayetuhumiwa kufanya mapenzi na mw... ...polisi

HABARI LEO UK 18

# * Vizimba vya ufugaji samaki 200 vyakamilika *

Na Abela Msikula, Mwanza

UJENZI wa vizimba 200 kati ya 615 vya ufugaji samaki katika Ziwa Victoria umekamilika.

Kadhalika boti 55 za uvuvi pamoja na vifaa vyake kama vile injini, nyavu, vifaa vya kutafutia samaki katika maji pamoja na maboya ya usalama navyo viko tayari.


Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega wakati wa ziara yake kukagua boti hizo na kuona maendeleo ya ujenzi wa vizimba.

Vizimba na boti ni sehemu ya Sh bilioni 25 ambazo ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB).

Ulega alisema takribani walengwa 2,000 Kanda ya Ziwa watanufaika na mradi huo ambao ni mkopo usio na riba, na mkopaji atatakiwa kumaliza marejesho ndani ya miaka minne.

"Lengo ni kukuza uvuvi kutoka tani 500,000 za samaki tunazovua sasa kwa mwaka, nchi nzima, hadi tani zisizopungua 700,000," alisema.

Mkurugenzi wa viumbemaji Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Nazael Madalla alisema jumla ya wanufaika wa mradi huo Kanda ya Ziwa ni vyama vya ushirika 93, kampuni 10 na watu binafsi 28.



wa uuzaji wa tumbaku hapa nchini, jambo Kingolwira mkoani Morogoro.

# Mahitaji makubwa ya maziwa fursa iliyo wazi nchini

Mainda Mhando, Mwananchi
mmhando@mwananchi.co.tz

Kila mwaka Tanzania hutumia Sh20 bilioni kwa ajili ya kuagiza lita za maziwa 20 milioni ili kukabiliana na upungufu wa maziwa nchini.

Uzalishaji wa maziwa kwa sasa ni lita 3.6 bilioni kwa mwaka, ambazo ni pungufu ya lita 9 bilioni zinazohitajika.

Upungufu huo umesababisha kwa mwaka 2022/2023 viwanda tisa vikubwa na vidogo vya kusindika maziwa kufungwa, huku vinavyoendelea kufanya kazi vikipata asilimia 30 tu ya mahitaji.

Vituo vya kukusanyia maziwa takriban 50 vimetajwa kutofanya kazi kutokana na upungufu huo.

Akizungumza na *Mwananchi*, katika mahojiano maalumu na Msajili wa Bodi ya Maziwa nchini, Dk George Msalya anasema unywaji mdogo wa maziwa ni miongoni mwa mambo yaliyochangia kuwapo kwa upungufu huo.

Anasema sababu za wananchi kutokufikia lengo la kunywa maziwa angalau lita 200 kwa mwaka linalopendekezwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) ni upungufu wa maziwa uliopo nchini.

"Maziwa yanayozalishwa kwa sasa ni robo ya mahitaji yetu, kwa hiyo bado uzingatiaji wa ulaji ni kidogo sana, kwa sasa kwenye ulaji tupo wastani wa lita 62 kwa mwaka kwa mtu mmoja.

> **"Kila jumatano ya mwisho wa mwezi wa tisa tumetenga kwa ajili ya siku ya unywaji maziwa shuleni na mwaka huu tutafanya Jijini Mwanza."**
>
> Dk George Msalya

Malengo yetu ndani ya kipindi cha 2025 tuwe tumefikia lita 64 kutoka lita 62 iliyopo sasa na angalau lita 100 ifikapo mwaka 2030," anasema Dk Msalya.

Pia, Dk Msalya anasema hali hiyo inachangiwa na uzalishaji duni wa maziwa kwa sababu asilimia 97 ya ng'ombe wanaofugwa nchini hufugwa kwa njia za kienyeji, hivyo kutoa maziwa kidogo.

Hata hivyo, anasema hadi sasa nchi ina idadi ya ng'ombe milioni 1.5 wa kisasa wanaotegemewa kutoa maziwa kwa wingi, hivyo idadi hiyo ni ndogo kwa uhitaji wa kiwanda kimoja kupata lita 250 kwa siku.

### Mkakati wa Serikali

Hivi sasa jitihada zinafanywa ili kufikia lengo la kila mtu kunywa maziwa kwa mwaka angalau lita 65 kufikia mwaka 2025 sanjari na kufufua viwanda vilivyokufa kwa sababu ya kukosa malighafi hiyo.

Dk Msalya anasema Wizara kwa kushirikiana na wadau wa mifugo nchini wanaendelea kutoa elimu kwa wafugaji kufuga kisasa ili kuleta mazao yenye tija, ikiwemo maziwa.

Anasema ili kuhakikisha upatikanaji, ukusanyaji na usindikaji wa maziwa nchini unaongezeka, Serikali ilitenga Sh4 bilioni mwaka 2022/23 na mwaka 2023/24 kwa ajili ya kuwekeza kwenye ujenzi wa vituo vya kukusanyia maziwa.

"Kwa upande wa uhimilishaji, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha ng'ombe wanafugwa kisasa ili kufikia kuzalisha lita 5 bilioni kufikia mwaka 2030," anasema.



Mwandishi wa Mwananchi, Mainda Mhando akifanya mahojiano na Msajili wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Dk George Msalya ofisini kwake jijini Dodoma. **Picha na Merciful Munuo.**

#### UBORA WA MAZIWA

**Akizungumzia tafiti zilizofanywa na Bodi ya Maziwa, Dk Msalya anasema sehemu za Ubungo (Dar es Salaam), Morogoro na Tanga zimebainika kuwa na maziwa yenye vimelea vya kusababisha magonjwa, hasa ya tumbo na kuharisha.**

**Anasema kati ya sampuli za maziwa zilizochukuliwa eneo la Ubungo Jijini Dar es Salaam, asilimia 80 ya sampuli hizo zimeonekana kuwa na vimelea vya magonjwa.**

**Dk Msalya anasema wadudu wa utupaji mimba wameonekana kuwepo kwa zaidi ya asilimia 30 katika maeneo ya Lushoto, mkoani Tanga na Mvomero, mkoani Morogoro.**

**Dk Msalya anawasihi wananchi wafuate kanuni kwa kununua maziwa bora ili kuepuka magonjwa yanayoambukiza kutoka kwa mnyama kwenda kwa binadamu.**

**Kanuni hizo ni kuzingatia usafi wa ukamuaji, uhifadhi, usafirishaji na usindikaji wa maziwa viwandani.**

Dk Msalya anasema jitihada hizo zinafanywa na Serikali ili kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuagiza maziwa kutoka nje na badala yake fedha hizo zitumike kwenye uzalishaji mali.

Aidha, Dk Msalya anasema bodi kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo inaendelea kuungana na wadau wa ndani na nje ya nchi kuimarisha upatikanaji wa maziwa, hasa katika jamii za pembezoni mwa miji.

Kuhusu suala la unywaji maziwa shuleni, Dk Msalya anasema bodi hiyo inazunguka maeneo tofauti nchini kuadhimisha siku hiyo ili kuwajengea uwezo wa kuendeleza programu ya unywaji maziwa.

Anasema Waziri wa mifugo amepewa dhamana ya kuteua mtu mmoja katika kila Halmashauri kusimamia sehemu zenye uhitaji wa maziwa shuleni kwa uharaka ili kupatiwe ufumbuzi.

Dk Msalya anatoa wito kwa wazazi, hususan katika shule za umma kuungana kwa pamoja kufanikisha programu ya unywaji maziwa shuleni ili kuondoa udumavu, njaa na kuongeza ari ya kujifunza na ufaulu shuleni.

### Unywaji maziwa shuleni bado

Kwa kutambua mchango wa lishe na wingi wa vitamini vinavyopatikana katika maziwa, Serikali ilianzisha siku ya unywaji maziwa shuleni mwaka 1996, lakini mwaka 2000 ndio utekelezaji ulianza rasmi.

"Ilipofika mwaka 2005 utekelezaji wake ulianza kwa kasi kwa sababu chombo rasmi cha kusimamia kilikuwa tayari kimeanzishwa na tangu hapo tunapiga hatua na lengo ni kufika nchi nzima," anasema.

Hata hivyo, siku ya unywaji maziwa shuleni ambayo inatekelezwa kila Jumatano ya mwisho wa mwezi, Septemba au Septemba 27 imeonekana kutofanya vizuri hasa katika shule za umma.

Dk Msalya anasema shule binafsi zinaendelea kufanya vizuri kwenye utekelezaji kwa sababu hutumia njia ya kuchangia kwa wazazi kununua maziwa kwa kipindi fulani shuleni, ukilinganisha na shule za umma ambazo zinategemea wafadhili.

Kwa mujibu wa bodi hiyo, ni mikoa sita tu yenye halmashauri 10 ambazo zinatekeleza utaratibu wa unywaji maziwa katika shule 55.

"Kwa upande wa shuleni tumeona fursa za kuwaongezea watoto hawa kasi ya ukuaji na kuondoa udumavu kwa sababu mtoto anapokuwa amedumaa inasababisha ukuaji, uelewa wake ni hafifu," anasema.